**HOTUBA YA WAZIRI MKUU MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE KONGAMANO LA KIKANDA LA BIASHARA NA UWEKEZAJI KATIKA TASNIA YA MAZAO YA BUSTANI LILILOFANYIKA KATIKA HOTELI YA THE KILIMANJARO HYATT REGENCY, DAR ES SALAAM, TAREHE 5 DESEMBA, 2020**

**SALAMU**

Ndugu Gerald Kusaya, Katibu Mkuu, Wizara ya Kilimo,

Mhandisi Zebadiah Moshi - Mwenyekiti wa TAHA,

Dkt. Jacqueline Mkindi - Afisa Mtendaji Mkuu wa TAHA,

Waheshimiwa Wabunge mliopo hapa,

Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Nchi Rafiki,

Wawakilishi wa kutoka nchi Wananchama wa Jumuiya za SADC na EAC

Wawakilishi wa Wizara na taasisi nyingine za Serikali,

Wageni Waalikwa,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

**Habari za Asubuhi!**

**SHUKRANI**

**Ndugu Washiriki,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uzima na kutukutanisha katika kongamano hili la Kikanda la Biashara na Uwekezaji katika Tasnia ya mazao ya Bustani.

**Aidha,** ninatoa shukrani zangu za dhati kwa waandaaji wa kongamano hili; Wizara ya Kilimo pamoja na TAHA kwa kunialika kuwa mgeni rasmi.

**Vilevile,** napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa washiriki wote kwa kutenga muda wenu na kujitokeza kwa wingi kushiriki katika kongamano hili muhimu sana kwa nchi yetu na Nchi za Jumuiya za EAC na SADC.

Ninaamini, kupitia kongamano hili wataalam wataweza kutafakari masuala mbalimbali yanayohusiana na biashara na uwekezaji kwenye tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani horticulture (yaani maua, viungo, matunda na mboga mboga) na jinsi gani tunaweza kutumia fursa zilizopo kwa maendeleo ya watu wetu. Hongereni sana TAHA kwa wazo zuri na maono haya.

**Ndugu Washiriki**, nitumie fursa hii pia kuwashukuru Wadau wa Maendeleo kwa michango yenu mikubwa kwenye maendeleo ya tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani.

Tunathamini sana mchango kutoka kwa Washirika wa maendeleo ambao wamekuwa wakifanya kazi bega kwa bega na Serikali yetu na kuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya Taifa letu.

**Kipekee**, nawashukuru Shirika la Kimataifa la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Swedeni (SIDA), Taasisi ya Maendeleo ya Uingereza, TradeMark East Africa, Serikali ya Ubelgiji, Shirika la kimataifa la maendeleo la Finland na Washirika wa maendeleo wengine kwa misaada mikubwa kwenye kuendeleza kilimo cha mazao ya bustani.

**Ndugu Washiriki,** kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba mpokee salamu na pongezi nyingi zenye heri na baraka kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mama yetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais. Viongozi wetu wamenituma nilete salamu na wameniambia kuwa wana imani kubwa kuwa kupitia kongamano hili la kikanda watanzania wataweza kunufaika na fursa mbalimbali za biashara za soko la ndani, kikanda na kimataifa. Vilevile kongamano hili litakuwa kivutio kwa wawekezaji kutoka nchi rafiki zikiwemo nchi za Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

## JITIHADA ZA KUENDELEZA KILIMO CHA MAZAO YA BUSTANI

Serikali inatambua kazi kubwa na jitihada zilizofanywa na TAHA kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuendeleza tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani. Maendeleo tunayoyaona leo kwenye hii tasnia ni kwa sababu ya jitihada zenu za kuwahudumia wakulima na wadau wengine. **Hongereni sana!**

**Kipekee**, niwashukuru sana TAHA, kwa kuwa ndiyo taasisi kiungo inayowahudumia wakulima wa mazao ya bustani kupitia program mbalimbali za kilimo cha mazao ya maua, viuongo, matunda na mbogamboga. Niwahakikishie kuwa Serikali inatambua na kuthamini juhudi na mchango wenu mkubwa katika kuendeleza tasnia hii. Endeleeni na jitihada hizohizo ili tuweze kuwakomboa wakulima wa nchi yetu. **Asanteni sana!**

### Ukuaji wa tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani

**Ndugu washiriki**, sote tumeshuhudia kwamba, tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani ina mchango mkubwa kwenye maendeleo ya uchumi hapa nchini. Kupitia tasnia hii tumepata manufaa mengi ikiwa ni pamoja na;

- kuwa mojawapo ya chanzo kikubwa cha ajira kwa watu zaidi ya milioni nne (4) na kuongeza kipato kwa Wakulima na Wafanyabiashara wengi hasa wale wa sokoni.
- Ongezeko la kipato kutokana na mazao ya bustani. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita uzalishaji wa mazao ya bustani nchini uliongezeka kwa asilimia 10.5 kutoka tani 5,931,900 mwaka 2015/16 hadi kufikia jumla ya tani 6,556,102 mwaka 2018/2019. Takwimu hizo zinathibitisha ukuaji wa tasnia hii na uwepo wa

haja ya kuweka mikakati ya kuiendeleza zaidi. Hivyo basi, kwa kuwa bei kwa tani inakadiriwa kuwa shilingi 500,000 thamani ya mazao ya kilimo cha mazao ya bustani kwa mwaka 2018/19 inakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi trilioni 3.3.

- tasnia hii inasaidia kujenga taifa lenye watu wenye afya nzuri na wenye nguvu na uwezo wa kufanya kazi. Sote tunafahamu kwamba, tasnia hii pia ni chanzo kikuu cha lishe na afya bora kwa Watanzania kutokana na virutubisho vingi kwa ulaji wa mbogamboga, matunda na viungo.

- mazao ya bustani yamekuwa na mchango mkubwa katika kupambana na gonjwa hatari la Covid-19. Dawa mbadala za asili zilizosaidia wananchi wengi duniani kote kudhibiti ugonjwa wa Corona zilitokana na matunda na viungo.

Kutokana na vilelezo hivyo, ni wazi kuwa mchango wa tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani kwenye maendeleo ya watu na uchumi wa nchi yetu na dunia kwa ujumla ni mkubwa na iwapo fursa zilizopo zitafanyiwa kazi, basi safari yetu ya kuelekea kwenye uchumi ulio imara zaidi itakuwa ya mafanikio makubwa, kwa kipindi kifupi.

## Ongezeko la Uhitaji wa Mazao ya Bustani Duniani

**Ndugu washiriki,** Uhitaji mkubwa wa mazao ya bustani kwenye masoko ya ndani, kikanda na kimataifa umesababisha mazao ya bustani kuwa biashara ya kimataifa tofauti na ilivyokuwa imezoeleka hapo awali kwamba mazao ya asili *(traditional crops)* ndiyo yaliyokuwa yanatawala masoko ya kimataifa.

Mathalan, takwimu za Shirika la Biashara Duniani za Mwaka 2020 zimebainisha kuwa, katika kipindi cha miaka mitano kati ya 2015 na 2019, biashara ya mbogamboga na matunda duniani ilikua kwa asilimia nne (4%) kutoka dola za Kimarekani bilioni 176 mwaka 2015 hadi dola za Kimarekani bilioni 206 mwaka 2019, ambalo ni ongezeko la dola bilioni 27.

Kwa upande mwingine, biashara ya mazao ya asili ilikua kwa asilimia moja (1%) tu toka dola za Kimarekani bilioni 240 hadi bilioni 246 ambalo ni ongezeko la bilioni 6 tu.

**Aidha,** katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, biashara ya baadhi ya mazao kama parachichi na viazi lishe imekua kwa asilimia kati ya asilimia 100 mpaka asilimia 200. Huu ni ushahidi wa uhitaji mkubwa wa mazao ya bustani hapa duniani. Hiyo ni fursa kubwa kwa wakulima, wafanyabiashara na wadau wengine wa tasnia hii kuichangamkia na kupata manufaa.

## Soko la mazao ya bustani ndani ya nchi

**Ndugu Washiriki,** suala la upatikanaji wa masoko ni muhimu sana ili kuifanya tasnia hii kuwa na mvuto mkubwa na kuchochea uzalishaji wa bidhaa. Inakadiriwa kuwa asilimia zaidi ya 90 ya mazao na bidhaa zote za mazao ya bustani zinazozalishwa hapa nchini huuzwa kwenye soko la ndani na kutumika na wa Tanzania.

Kwa idadi ya watu milioni 56, Tanzania inahitaji tani 8,135,120 za mbogamboga na matunda kwa mwaka, Takwimu hizi ni kutokana na mahitaji ya virutubisho na kumwezesha kila Mtanzania ale kilo 146 za mazao hayo kwa mwaka kama inavyoshauriwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula Duniani *(UN Food and Agriculture Organization – FAO).* Kutokana na kasi ya ukuaji wa watu, uhitaji huu utaongezeka hadi kufikia tani milioni 11 mwaka 2024. Takwimu hizo zinathibitisha ukubwa wa soko la ndani la mazao ya bustani.

**Soko la mazao ya bustani Ukanda wa EAC na SADC**

**Ndugu Washiriki**, kama inavyofahamika, Tanzania ni Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika*.* Nchi hizi zina wanachama 21 na idadi ya watu ipatayo milioni 500 sawa na asilimia 36.2 ya watu wote waliopo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tanzania imezungukwa na nchi nane ambazo ni Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, DRC, Msumbiji, Zambia na Malawi.

Nchi hizi kwa pamoja zina idadi ya watu inayokadiriwa kuwa milioni 274 ambayo ni sawa na asilimia 57 ya watu wote waliopo katika nchi za EAC na SADC. Taswira tunayoipata hapa ni kuwa kuna fursa kwa Taifa letu la Tanzania kulisha watu milioni 274 ambao ni majirani zetu wanaotuzunguka, lakini pia kuwafikia watu wengine milioni 274 ambao nchi zao zinafikika kiurahisi kutokea Tanzania.

**Ndugu Washiriki,** takwimu kutoka vyanzo mbalimbali zinaonesha kuwa nchi wanachama wa EAC na SADC zimekuwa zikiagiza kutoka nje kiasi kikubwa cha mbogamboga, matunda, viungo na bidhaa zinazotokana na usindikaji wa mazao husika.

Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2015 hadi 2019, nchi za EAC na SADC ziliagiza mbogamboga na matunda yenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 6.6 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania trilioni 15.2 za kitanzania Katika kipindi hicho, nchi hizi zimekuwa zikitumia wastani wa dola za Kimarekani bilioni 1.3 sawa na shilingi trilioni 3.04 za Tanzania kila mwaka kuagiza mazao na bidhaa mbalimbali zinazotokana na kilimo cha mazao ya bustani.

**Aidha,** katika kipindi cha miaka mitatu tu kati ya 2015 na 2018, uagizaji wa mazao hayo kutoka nchi wanachama wa Jumuiya hizi umeongezeka kwa asilimia 24.2. Takwimu hizo zinathibitisha kuongezeka kwa matumizi ya mbogamboga, matunda, viungo na bidhaa zilizosindikwa kunakoambatana na kukua kwa kasi kwa biashara ya nje kwa mataifa ya SADC na EAC.

**Uhitaji wa bidhaa zitokanazo na mazao ya bustani zilizosindikwa**

**Ndugu Washiriki,** kama nilivyotangulia kusema hapo awali, fursa za biashara zinazoambatana na uwekezaji katika tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani ndani ya Jumuiya zetu haziishii kwenye mazao mabichi (fresh produce) peke yake, bali pia bidhaa zilizosindikwa. Bidhaa za matunda na mbogamboga zilizokaushwa, maji ya matunda (juisi) na unga wa mboga na viungo zina uhitaji mkubwa kwenye nchi zetu na soko la dunia kwa ujumla.

- Katika mwaka 2019 peke yake, nchi za EAC na SADC zilinunua toka nje bidhaa aina ya maji ya matunda zenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 291. Ipo haja ya sisi kama nchi kuongeza uzalishaji wa aina mbalimbali za matunda na mbogamboga kama maembe, nyanya, parachichi na machungwa. Hii itasaidia kuondokana na utegemezi mkubwa wa malighafi kutoka nje na kukuza uzalishaji katika viwanda vya ndani.

**Faida ya kuongeza mavuno yanayotokana na kilimo cha mazao ya bustani**
**Ndugu Washiriki**, licha ya nchi yetu kuwa na fursa za kuzalisha na kusindika karibu kila aina ya mazao hapa nchini kutokana na kuwa na hali nzuri ya hewa, udongo mzuri na miinuko tofauti kutoka usawa wa bahari, pamoja na fursa zilizopo na biashara kubwa inayoendelea kufanyika katika Jumuiya zetu, ushiriki wetu Tanzania bado ni mdogo. Kwa wastani, tunauza mazao kwenye nchi zote hizo yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 20 tu kwa mwaka sawa na asilimia1.5 ya thamani ya mazao yote yanayoagizwa na nchi za EAC na SADC.

Ili tuweze kupata manufaa zaidi ya mtangamano wa EAC na SADC, hatuna budi kuchukua na kutekeleza hatua thabiti za kuongeza ushindani wetu kwenye masoko ya kikanda, lakini pia na yale ya Kimataifa. Uwezo wa kuongeza mavuno katika kilimo chetu ni mbinu pekee ya kuingia katika soko la ushindani kikanda na kimataifa. Suala hili litawezekana kwa kuwapa mbinu na maarifa Wakulima wetu pamoja na teknolojia zinazoweza kuwapa mafanikio ya kupata mavuno mengi ya kutosha ili kupata manufaa zaidi kutokana na shughuli za kilimo.

**Mavuno ya zao la nyanya**
Wakulima wetu wengi wakilima ekari moja ya nyanya hupata mavuno ya tenga 50 hadi 200 tu kwa msimu. Katika miezi kati ya Juni na Agosti kila mwaka, bei ya nyanya kwa tenga hushuka sana hata kufikia shilingi elfu saba na kwa bei hii, ni vigumu kwa mkulima anayevuna chini ya tenga 200 za nyanya kupata faida. Lakini, naambiwa na wataalam kuwa mkulima mwenye maarifa ya kutumia mbinu na teknolojia bora anaweza kuvuna tenga 500 hadi 800 kwenye ekari moja. Ni dhahiri kuwa mkulima anayepata mavuno kiasi hicho anaweza kupata faida hata kama anauza tenga moja kwa shilingi 5,000.

**Mavuno ya zao la kabichi**
Katika kilimo cha zao la kabichi wakulima wengi huvuna kabichi 3,500 - 5000 kwenye ekari moja, wakati watakapolima kitalaam, wanaweza kuvuna kabichi kuanzia 18,000 – 20,000 ambayo ni karibu mara nne ya mavuno ya kawaida. Kwa mavuno haya, hata akiuza kabichi moja shilingi 150 bado mkulima atapata faida na akipata bei nzuri anaweza kutajirika ndani ya msimu mmoja. Mifano ya aina hii tunaiona pia kwenye mazao mengi mengine.

**Ndugu Washiriki,** nichukue nafasi hii kutoa wito kwa Wizara ya Kilimo, TAHA na wadau wengine kuongeza jitihada za kuwapa maarifa na ufahamu wakulima wa kilimo cha mazao ya mbogamboga, viungo, maua na matunda ili kuongeza uwezo wa Tanzania kushindana kwenye masoko ya kimataifa.

**Mchango wa mazao ya bustani katika kukuza uchumi uzoefu kutoka mataifa mbalimbali.**
Suala la kuleta mapinduzi ya kijani kupitia tasnia ya kilimo cha mazao bustani halikwepeki. Uzoefu unaonesha kuwa zipo baadhi ya Nchi ambazo maendeleo ya uchumi wake yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na tasnia ya kilimo cha mazao bustani na wameweza kupiga hatua kubwa za maendeleo. Mifano hiyo ni pamoja na:

- **Kenya**: Katika mwaka 2019 nchi jirani ya Kenya imeingiza dola za kimarekani bilioni 1.37 kupitia tasnia hii ya mazao ya bustani.

- **Ecuador**; Katika mwaka 2019 peke yake, nchi hii iliingiza dola za Kimarekani bilioni tatu kama pato la kigeni kutokana na mauzo ya ndizi.

- **Mexico**; iliingizia nchi dola za Kimarekani bilioni 2.8 kutokana na uzalishaji wa tani milioni 2 nchini za zao la parachichi.

- **Misri**; bidhaa ya machungwa iliwaingizia dola za Kimarekani milioni 748 mwaka 2019 na mbogamboga kwa ujumla dola bilioni moja.

Aidha, uchumi wa nchi za **Ufilipino** na **Costa Rica** nao unachangiwa sana na zao la ndizi. Mazao yote hayo niliyoyataja yanaweza kuzalishwa Tanzania, tena kwa wingi zaidi kuliko nchi nyingi zikiwemo nilizotolea mifano.

**MIKAKATI YA KUSHUGHULIKIA CHANGAMOTO ZA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA KILIMO**

**Ndugu Washiriki**, Serikali ipo tayari wakati wote kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazohusiana na mazingira ya biashara kwa nia ya kufanya maboresho. Tunatambua kuwa mazingira wezeshi ya biashara ni muhimu katika kuleta maendeleo ya tasnia ya mazao bustani.

**Kufuta kodi na tozo zinazohusu sekta ya kilimo**

Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, imepunguza na kufuta kodi na tozo 168 ambapo 114 zilihusu sekta ya kilimo na tasnia ya mazao ya bustani ikiwa miongoni mwa wanufaika wakubwa. Hatua hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa pembejeo, zana za kilimo na huduma zinapatikana kwa wingi na kwa bei ambazo wakulima na wadau wengine wanazimudu.

**Kuimarisha Miundombinu ya Usafirishaji wa Mazao**

**Ndugu Washiriki**, suala la usafirishaji ni la msingi katika kuwezesha biashara hususan ya mazao yanayoharibika haraka kama mazao ya bustani, minofu ya samaki na nyama. Na niwafahamishe kupitia kongamano hili kuwa serikali inatambua uwepo wa changamoto katika usafirishaji wa bidhaa.

Serikali chini ya uongozi thabiti wa Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli imeweka mikakati mbali mbali ya kuboresha miundombinu nchini kwa kufanya yafuatayo:

**Moja:** Kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020 - 2025, imeweka bayana mpango wa kuboresha mazingira ya usafirishaji wa bidhaa zinazoharibika haraka kwa kununua ndege ya mizigo kwa kuzingatia mahitaji ya biashara na ukuaji wa uchumi. Pamoja na ndege ya mizigo tutanunua ndege kubwa mbili za masafa marefu na ndege mbili za masafa ya kati ili kuongeza fursa za biashara.

**Mbili:** Serikali imeshaunda kamati maalum inayojumuisha wataalamu wa serikali na wale wa sekta binafsi. Kamati hiyo imeanza kuainisha changamoto za usafirishaji na za kimfumo katika bandari na viwanja vyetu vya ndege ili kufanya maboresho yanayohitajika na hivyo tuweze kutumia miundombinu ya ndani katika kusafirisha bidhaa zetu.

**Ndugu Washiriki**, nitumie fursa hii kuziagiza taasisi zote zinazohusika na usafirishaji wa mizigo kwa njia ya anga na bahari pamoja na Kamati iliyoundwa kusimamia zoezi hili kwa ukamilifu. Hii ni pamoja na kufanyia kazi kwa haraka mapendekezo ya wataalamu yatakayotokana na utafiti unaoendelea kuhusu kuboresha miundombinu na mifumo ya usafirishaji.

## UIMARISHAJI WA MASOKO YA MAZAO YA BUSTANI

**Ndugu Washiriki,** mtakumbuka kuwa katika muhula wa kwanza wa Serikali hii, mwelekeo ulikuwa zaidi kwenye kujenga uchumi wa Viwanda. Katika kipindi hiki, mpango utajielekeza zaidi kwenye kuupeleka uchumi wetu kuwa kupitia tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani itakayo kuwa na mchango mkubwa kwenye kufanikisha malengo ya Mpango huu kutokana na fursa za masoko ambazo nimekwishazitaja.

**Nimefurahi kusikia kwamba,** wadau wa mazao ya mbogamboga na matunda wakiongozwa na TAHA wanashirikishwa kikamilifu kwenye uandaaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021 – 2025). Ni matumaini yangu kuwa masuala kama haya ya masoko ya kikanda ambayo yanajadiliwa kwa kina leo yatakuwa sehemu ya Mpango huo.

Vilevile, Serikali itaendelea kushirikiana Sekta binafsi kuandaa mkakati wa kitaifa wa kuyafikia masoko mbalimbali. Natoa wito kwa taasisi za Serikali, wadau wa Maendeleo na wadau wengine wote kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa mipango hiyo pindi itakapokuwa tayari kwa utekelezaji kuanzia mwaka ujao wa fedha.

## Kuboresha Mifumo ya Utoaji Huduma

**Ndugu Washiriki,** Serikali imeanzisha Mamlaka ya Dawa na Afya ya Mimea Tanzania **(Tanzania Pesticides and Plant Health Authority – TAPHA)** ambayo imejumuisha shughuli zote zinazohusiana na ukaguzi na usajili wa mimea na dawa. Lengo ni kuboresha mifumo ya kitaasisi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi katika

kuhakikisha kuwa wakulima wanapata pembejeo na huduma za kuongeza tija ya kilimo.

**Mikakati ya kutafuta fursa za masoko ya mazao ya bustani**

**Ndugu Washiriki**, ni vema wote tukatambua umuhimu wa kuongeza jitihada za kupanua wigo wa masoko. Suala la kutafuta masoko lijadiliwe kwa mapana yake. Ni dhahiri kuwa zipo fursa nyingi na bado hazijafanyiwa kazi. Zipo fursa ambazo zinapatikana kwenye mikataba yetu na nchi nyingine (bilateral agreements*)* na fursa kupitia Mpangilio Maalum wa biashara ya upendeleo *(*preferential trade arrangements).

**Ndugu Washiriki,** kwa mara nyingine niwapongeze Wizara ya Kilimo na TAHA kwa jitihada mnazozifanya ili kuimarisha masoko ya mazao. Nimeelezwa kuwa Mwaka 2015, Wizara yetu ya Kilimo ilishirikiana na TAHA kujenga miundombinu ya masoko kikiwemo Kituo cha kukusanyia mazao kule Njombe na matokeo yake tumeyaona ndani ya muda mfupi baada ya kuanza kufanya kazi mwaka 2017.

Kituo hiki, kimekuwa kikiwahudumia wakulima wa parachichi ambapo hadi kufikia mwezi Agosti mwaka huu, jumla ya tani 540 ziliuzwa kwenda masoko ya nje na kuiingizia nchi kiasi cha dola za Kimarekani milioni moja. Mazao hayo yalinunuliwa kwa wakulima 840, waliojiingizia kipato cha shilingi milioni 759. Hongereni sana kwa jitihada za kuinua kipato cha wakulima.

**MAAGIZO NA MASUALA YA MSISITIZO**

- Kutokana na matokeo chanya kufuatia ujenzi wa Kituo cha kukusanyia mazao kule Njombe, nitoe wito kwa Wizara ya Kilimo, TAHA pamoja na wadau wengine wa tasnia hii kuanisha maeneo ya kimkakati katika uzalishaji wa mazao ya bustani na kuanzisha vituo vya ukusanyaji mazao hayo hususan maeneo ya vijijini na mipakani. Ujenzi wa vituo vya kukusanyia mazao utaleta mafanikio makubwa kwa wakulima katika kipindi kifupi.

- Wizara ya Kilimo shirikianeni na wadau wa tasnia hii kuuhisha na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kuendeleza kilimo cha mazao ya bustani. Aidha, TAHA na wadau wote wa tasnia hii hakikisheni mipango inaendana na malengo na programu za serikali kupitia mkakati unaotekelezwa.

- Wizara ya Kilimo anzisheni Mamlaka ya Horticulture itakayosimamia mazao ya matunda na mbogamboga tu kama ilivyo kwa nchi jirani za Kenya, Ethiopia, Rwanda nk.

- Wizara za Kilimo, Fedha na Mipango na Viwanda na Biashara wekeni utaratibu wa kutambua zao la AVOCADO linalosafirishwa na nchi jirani litambulike kuwa linazalishwa hapa nchini;

- Kwa upande wa TAHA wekeni mpango wa kuwafikia, kuwaunganisha na kuwawezesha wakulima wadogo wa mazao ya bustani hasa waliopo vijijini kuandaa bidhaa bora na kupata masoko ya bidhaa zao. Jitihada zenu zisiishie katika

makampuni makubwa tu kwani wakulima wadogo nao wanao mchango mkubwa katika ukuzaji uchumi wetu.

- Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Viwanda na Biashara fanyeni kikao cha pamoja na wadau wa tasnia hii kuanisha aina ya vifungashio vinavyokidhi viwango vya biashara ya mazao ya bustani kwa soko la ndani na soko la kimataifa. Aidha, Wizara ya Viwanda iweke mkakati wa kuitangaza fursa ya uanzishaji wa viwanda vya vifungashio hapa nchini.

- Wizara ya Kilimo anzisheni kituo cha utafiti cha mazao ya matunda na mbogamboga ili kiweze kuyatambua kwa kupata takwimu na kufanya utafiti ili kukidhi mahitaji ya uzalishaji

- Wizara ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Kilimo hakikisheni mnashirikiana na wadau wote muhimu ikiwemo TAHA kupitia na kuchambua Mikataba yote tuliyo nayo na nchi nyingine, ili kutafsiri fursa za masoko ya mazao ya bustani na mazao mengine. Aidha wekeni mpango mkakati wa kuzitumia fursa hizo.

- Wizara ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Balozi zetu fanyeni tafiti kubaini nchi ambazo zina fursa kubwa ya upatikanaji wa masoko ya mazao ya bustani lakini hatuna mikataba nazo.

Nafahamu sisi kama nchi hatujaweza kufaidika na fursa nyingi za masoko ya nje ikiwamo na mipango kama ule wa African Growth Opportunity Act (AGOA), licha ya fursa nyingi zilizopo katika soko la Marekani.

## WITO KWA WAWEKEZAJI

**Ndugu Washiriki,** Serikali inathamini mchango wa sekta binafsi katika kukuza uchumi na imekuwa ikishirikiana nayo katika nyanja mbalimbali. Pia, imekuwa ikiimarisha mifumo mbalimbali ili kujenga mazingira rafiki ya biashara.

**Hivyo basi**, kwa niaba ya Serikali, nitumie nafasi hii kuwakaribisha wawekezaji kutoka barani Afrika na kwingineko kuja kuwekeza nchini Tanzania kwani tuna vivutio vingi vya uwekezaji ikiwemo ardhi ya kutosha, maji, nishati ya umeme, hali ya hewa nzuri kabisa, miundombinu ya usafirishaji na soko la ajira lenye ushindani.

Yapo maeneo mengi mnayoweza kuwekeza nchini Tanzania katika sekta yetu ya kilimo na hasa mazao ya bustani. Niwahakikishie kuwa*,* Serikali itaendelea kufanya kazi na sekta binafsi, kutatua kwa wakati changamoto zinazowakabili ili kujenga mazingira rafiki ya kufanya biashara.

## HITIMISHO

**Ndugu washiriki,** nihitimishe kwa kutoa wito kwenu nyote mtumie fursa hii vizuri kujadiliana kuhusu namna bora ya kuzifanyia kazi hizi fursa za uwekezaji na biashara zilizopo na hivyo kufikia malengo ya kongamano hili. Nasubiri kwa hamu kubwa kusoma taarifa ya kongamano na kuona mikakati na maazimio mtakayokubaliana.

Kwa maneno haya machache, natamka kwamba **Kongamano la Kikanda la uwekezaji katika Tasnia ya mazao ya bustani limefunguliwa** rasmi.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA!**

**MUNGU IBARIKA NA AFRIKA!**